# THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

**KISWAHILI LUGHA**
**School Based Assessment**
**Gredi ya 10**
**Muda: Wiki 4**

**JINA la Mtathminiwa:** ____________ **Nambari ya Tathmini :** _____________

**JINA la Shule:** ____________________________ **Sahihi:** __________________

**Maagizo**

a) Tathmini hii ina mazoezi **Sita**.
b) Kila zoezi lina maagizo yake.
c) Zoezi la 1 na 2 litafanywa kwa ushirikiano wa mwanafunzi na Mwalimu. (Ana kwa ana)
d) Mazoezi haya yafanywe kwa muda wa wiki 4.

**Alama: 80**

| **Kwa Matumizi ya Mtathmini Pekee** | | **Alama** | |
|---|---|---|---|
| **1** | **Kusikiliza** | **10** | |
| **2** | **Kuzungumza** | **20** | |
| **3** | **Kuandika** | **20** | |
| **4** | **Tafsiri** | **10** | |
| **5** | **Ufupisho** | **10** | |
| **6** | **Kuhariri Matini** | **10** | |
| **Jumla** | **80** | **80** | |

SAMPLE TASKS

*© 2025 The Kenya National Examinations Council.*

**Maagizo kwa Mtathminiwa**

1. Karatasi hii ya maswali ina **Mazoezi matano:**

| | |
|---|---|
| **ZOEZI 1:** Kusikiliza na Kuzungumza | (10) |
| **ZOEZI 2:** Kuzungumza | (20) |
| **ZOEZI 3:** Kuandika | (20) |
| **ZOEZI 4:** Tafsiri | (10) |
| **ZOEZI 5:** Ufupisho | (10) |
| **ZOEZI 6:** Kuhariri Matini | (10) |

2. Jibu maswali kulingana na maagizo ya kila zoezi.

**Maagizo kwa Mwalimu**

1. Kila zoezi lina mwongozo wa kutathminia.
2. Tumia fomu ya kutathminia kila mwanafunzi kutathminia utendaji wa mwanafunzi.
3. Hakiki umilisi unaolengwa kwa kutumia orodha hakiki uliyopewa.

SAMPLE TASKS

**ZOEZI LA 1**

**KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA** **(alama 10)**

**Maelezo kuhusu zoezi:**

Zoezi linalenga kutathmini **uwezo wa mawasiliano bora**, unaojumuisha:

- Kusikiliza kwa makini na kuelewa ujumbe,
- Kuzungumza kwa ufasaha, uwazi, na adabu,
- Kutumia lugha ya Kiswahili sanifu kwa ufanisi katika mazingira mbalimbali.

**Jibu swali la 1 au 2**

**1.** (a). Tazama na kusikiliza kwa makini video iliyomo kwenye kiungo kifuatacho kisha ujibu maswali
https://youtu.be/Euao4nzxKFM

i. Mabadiliko ya tabianchi yanahusu nini? (alama 3)
ii. Eleza kwa aya moja mambo yanayosababisha mabadiliko ya tabianchi.
iii. Eleza maana ya:

a) Mionzi ya jua (alama 1)
b) Kongamano (alama 1)

(b). Teknolojia imechangia vipi mabadiliko ya tabianchi? Eleza kwa hoja **tano.** (alama 5)

**AU**

2. Tazama na kusikiliza kwa makini video ifuatayo kisha ujibu maswali
https://youtu.be/R2IzihUvyIg
a) Ni nini kilichosababisha msongamano wa magari. (alama 2)

b) Eleza umuhimu wa tukio lililosababisha hali hiyo nchini. (alama 3)
c) Tatizo la msongamano wa magari katika barabara za jiji la Nairobi linaweza kutatuliwa vipi? Eleza. (alama 5)

**Tanbihi:** *Mwalimu anaweza kumwuuliza kila mmoja kujibu moja kwa moja maswali hayo pasi na mwanafunzi kuandika majibu yake. Aidha mwanafunzi anaweza kuandika majibu kwenye daftari.*

**ZOEZI LA 2** **(alama 20)**

**KUZUNGUMZA**

**Maelezo kuhusu zoezi:**

Zoezi hili ni la kutathmini umilisi wa mwanafunzi wa kuzungumza kwa ufasaha kuhusu suala fulani. Zoezi hili pia litatumika kutathmini umilisi wa mwanafunzi wa kujithamini.

**MAAGIZO**

Mwanafunzi achague swali la **1** au la **2.**

**1.**

a) Umepewa kadi **nne** zenye mada mbalimbali.
b) Chagua kadi moja kisha ufanye yafuatayo:
   i. Kwa muda wa dakika 10 andika hoja ambazo utawasilisha kwa mtathmini nafasi yako ikifika.
   ii. Katika wasilisho lako hakikisha umeanda slaidi ambazo utatumia.
   iii. Katika wasilisho lako utatathminiwa kwa yafuatayo
      a) Uelewa wa mada.
      b) Ufasaha wa kuzungumza.
      c) Kasi ya uzungumzaji
      d) Matumizi ya ishara za mwili
      e) Matumizi ya lugha.

**KADI A**

Jamii ina uwezo wa kutatua tatizo la ukosefu wa chakula kupitia mbinu za kilimobora. Jadili.

**KADI B**

Elimu ya umilisi ina umuhimu mkubwa katika maendeleo ya taifa nchini kenya. Jadili.

**KADI C**

Jamii inafaa kuhamasishwa kuhusu lishe bora. Jadili.

SAMPLE TASKS

**KADI D**

Mtoto anafaa kulindwa dhidi ya unyanyaswaji. Fafanua.


## AU

2. Teua picha mojawapo ya zifuatazo kisha ubuni mada kuhusiana na picha uliyoteua. Jadili kwa muda wa **dakika mbili** suala au masuala yanayoibuliwa. Ubunifu na uasilia wako utazingatiwa katika kuhakiki uwasilishaji na kiwango chako cha kufaulu.











**ZOEZI LA 3** **(alama 20)**

**Maelezo kuhusu zoezi**

Lengo kuu ni **kuchunguza uwezo wa mwanafunzi kuwasilisha mawazo kwa maandishi** kwa kutumia lugha ya Kiswahili sanifu, kwa uwazi, mpangilio, ubunifu na ufasaha. Aidha zoezi hili linalenga kupima umilisi wa mwanafunzi wa kuandika tungo za kiuamilifu. Kupitia zoezi hili umilisi wa kidijitali utazingatiwa pale mwanafunzi anapopiga chapa kazi yake na kuisambaza kupitia kwa baruapepe. Uwezo wa mwanafunzi wa kuzingatia maagizo utatiliwa maanani.

**KUANDIKA**

1. Mwandikie mhariri wa Gazeti la *Mulika* makala yatayochapishwa kwenye Gazeti kuhusu umuhimu wa kutunza mazingira. Makala yako yasipungue maneno 200.
   Makala hayo yapigwe chapa kwa kutumia kifaa cha kidijitali. Baadaye yatume kwa kutumia pepe ya mwalimu baraka@gmail.com

**ZOEZI LA 4: TAFSIRI**

**Maelezo kuhusu zoezi**

Lengo la zoezi hili tafsiri ni kumsaidia mwanafunzi kukuza uelewa wa lugha na mawasiliano kati ya lugha mbili. Kupitia tafsiri, mwanafunzi ataweza:

i. Kuelewa maana kamili ya maandishi katika lugha chanzi (asili).
ii. Kuchagua maneno sahihi ili kufikisha ujumbe uleule kwa lugha lengwa.
iii. Kuimarisha ufasaha na msamiati katika lugha zote mbili.
iv. Kuthamini tamaduni na mitazamo tofauti iliyomo katika lugha.
v. Kukuza umakinifu na fikra pevu katika kuchambua maana ya maneno na mitindo ya uandishi.

**(Alama 10)**

**TAFSIRI**

*Soma matini ifuatayo ya Kiingereza kisha utafsiri kwa lugha ya Kiswahili*

Road accidents are a major cause of injuries and deaths across the world. One of the leading causes is careless driving, such as overspeeding, overtaking dangerously, and ignoring traffic rules. Many accidents also occur because of drunk driving, where drivers lose control due to impaired judgment. Another cause is the use of mobile phones while driving, which distracts attention from the road. Poor road conditions, such as potholes and lack of proper signage, also contribute to accidents. Additionally, unroadworthy vehicles and failure to maintain them properly can lead to mechanical failures that cause crashes.

SAMPLE TASKS

To prevent road accidents, both drivers and authorities must play their part. Drivers should always follow traffic rules, avoid speeding, and never drive under the influence of alcohol or drugs. They should also keep their vehicles in good condition and stay alert while driving. Authorities, on the other hand, should ensure that roads are well maintained, install clear signs, and enforce traffic laws strictly. Regular public awareness campaigns about road safety can also help change negative attitudes towards safe driving. By combining responsible behavior and strict enforcement, the number of road accidents can be significantly reduced, making roads safer for everyone.

**JIBU:**

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

**ZOEZI LA 5 : UFUPISHO** **(Alama 10)**

Zoezi hili litamwezesha mwanafunzi kuchambua na kuwasilisha mawazo muhimu kwa ufasaha na kwa maneno machache.

Kupitia ufupisho, mwanafunzi ataweza:

i. Kutambua hoja kuu na maelezo muhimu katika maandiko.
ii. Kuondoa taarifa zisizo na umuhimu bila kupoteza maana.
iii. Kujieleza kwa uwazi, mpangilio na umakinifu.
iv. Kuimarisha uelewa wa kusoma na kuandika kwa muhtasari.

**UFUPISHO**

*Soma matini ifuatayo kisha ujibu maswali*

Ajali za barabarani ni chanzo kikuu cha majeraha na vifo duniani. Mojawapo ya sababu kuu ni uendeshaji mbaya wa magari kama vile mwendo wa kasi kupita kiasi, kuyapita magari mengine kwa njia hatari, na kutokufuata sheria za barabarani. Ajali nyingi pia hutokea kutokana na ulevi wa madereva, ambapo hushindwa kudhibiti magari kwa sababu ya kuhisi vibaya au kupoteza umakini. Sababu nyingine ni matumizi ya simu wakati wa kuendesha gari, jambo linalosababisha madereva kutokuzingatia barabara. Hali mbaya ya barabara kama mashimo na ukosefu wa alama sahihi za barabarani pia huchangia ajali. Aidha, magari yasiyokuwa katika hali nzuri na kushindwa kuyatunza ipasavyo yanaweza kusababisha hitilafu za kiufundi zinazoleta ajali.

SAMPLE TASKS

Ili kuzuia ajali za barabarani, madereva na mamlaka husika wanapaswa kushirikiana. Madereva wanapaswa kufuata sheria za barabarani, kuepuka mwendo wa kasi, na kutoendesha wakiwa wamelewa pombe au dawa za kulevya. Pia wanapaswa kuhakikisha magari yao yako katika hali nzuri na kuwa makini wanapokuwa barabarani. Kwa upande mwingine, mamlaka zinapaswa kutengeneza barabara ipasavyo, kuweka alama wazi, na kutekeleza sheria kwa ukali. Kampeni za uhamasishaji kuhusu usalama barabarani zinaweza kusaidia kubadilisha mitazamo hasi. Kwa kushirikiana kwa uwajibikaji, idadi ya ajali inaweza kupunguzwa kwa kiasi kikubwa na barabara kuwa salama kwa wote.

a) Fupisha ujumbe wa matini hii kwa maneno 65

b) Eleza msimamo wa mwandishi kwa maneno 20

**ZOEZI LA 6 : KUHARIRI MATINI** **(Alama 10)**

Lengo la zoezi la kuhariri kwa mwanafunzi ni kumwezesha kuboresha maandishi kwa kuyasahihisha na kuyapamba ili yawe sahihi, wazi na yenye mpangilio mzuri.

Kupitia uhariri, mwanafunzi ataweza:

1. Kugundua na kusahihisha makosa ya kisarufi, tahajia na alama za uandishi.
2. Kuboresha mtiririko na mpangilio wa mawazo.
3. Kuchagua maneno sahihi na mtindo unaofaa.
4. Kuzingatia umbo na ufasaha wa maandishi.

**KUHARIRI MATINI**

**MAAGIZO**

1. *Soma matini ifuatayo kwa makini.*
2. *Iandike upya kwa kurekebisha makosa yaliyomo.*
3. *Zingatia ujumbe uliolengwa unapohariri matini hii.*

Ajali za barabarani husababiswa na mwendo wa kasi sana ulevi wa madereva na matumizi ya runinga  wakati wa kuendesha. Barabara nyingi ni mbovu sana kwa sababu serikali haijali kutengeneza Madereva wanastahili kufwata sheria na kuhakikisha Magara yawo iko salama. Serikari inafaa kuweka alama za barabara wazi kabisa na kuelimisha wanainchi kuhusu usalama wa barabarani ili kupunguza ajali ambazo zinasababisha vifo vingi sana kila siku.

SAMPLE TASKS

Wajibu wangu katika kuhakikisha usalama barabarani ni kufuata sheria za barabarani na kuwa mwangalifu ninapotumia barabara.

**JIBU**

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA**

SAMPLE TASKS

THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

# MWONGOZO WA KUTATHMINIA
# KISWAHILI LUGHA
# GREDI YA 10

SAMPLE TASKS

**MWONGOZO HUU UNA KURASA 20 ZILIZOPIGWA CHAPA.**

# ZOEZI LA 1: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

**Vipengele vya Kutathmini Kusikiliza**

**Lengo Kuu**

Kutathmini **uwezo wa mawasiliano bora**, unaojumuisha:

- Kusikiliza kwa makini na kuelewa ujumbe,
- Kuzungumza kwa ufasaha, uwazi, na adabu,
- Kutumia lugha ya Kiswahili sanifu kwa ufanisi katika mazingira mbalimbali.

| Kipengele | Maelezo | Viwango vya Ufasaha |
|---|---|---|
| 1. **Uelewa wa ujumbe** | Mwanafunzi anaelewa kwa usahihi yale anayoyasikia. | - Anapata maana kuu na maelezo madogo<br>.- Anaweza kueleza upya alichosikia. |
| 2. **Umakini na usikivu** | Anaonyesha dalili za kufuatilia hotuba, mjadala, au simulizi. | - Hutazama mzungumzaji, huuliza maswali, na hurejelea hoja sahihi. |
| 3. **Uwezo wa kuchambua** | Anaweza kutofautisha hoja, maoni na hisia katika hotuba. | - Hutambua msisitizo, sauti, na lengo la msemaji. |
| 4. **Uwezo wa kutoa mrejesho** | Anaweza kujibu kwa usahihi maswali au kutoa maoni baada ya kusikiliza. | - Majibu yake yanaonyesha uelewa wa ujumbe. |

## Jedwali la Kutathmini Ujuzi wa Kusikiliza na Kuzungumza

| Kipengele | Maelezo ya Kinachotathminiwa | 5 (Bora sana) | 4 (Nzuri) | 3 (Wastani) | 2 (Duni) | 1 (Haitoshi) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **1. Uelewa wa ujumbe** | Kuelewa maana kuu na maelezo madogo ya anachokisikia | Anaelewa ujumbe wote kwa usahihi | Anaelewa sehemu kubwa | Anaelewa ujumbe kwa jumla tu | Anaelewa sehemu ndogo | Haelewi ujumbe kabisa |
| **2. Umakini wa usikivu** | Kuonyesha ufuatiliaji na tahadhari wakati wa kusikiliza | Huonyesha makini kila wakati | Huwa makini mara nyingi | Huwa makini kiasi | Huwa hajali mara kwa mara | Hupoteza umakini kabisa |
| **3. Uwezo wa kuchambua** | Kubaini hoja, hisia, au lengo la msemaji | Hutambua hoja zote na kuzifafanua | Hutambua hoja nyingi | Hutambua hoja kuu pekee | Hupata hoja chache | Hawezi kuchambua ujumbe |
| **4. Utoaji wa mrejesho** | Kujibu au kutoa maoni baada ya kusikiliza | Majibu sahihi na yenye hoja | Majibu sahihi kwa sehemu | Majibu yasiyo na kina | Majibu ya kubahatisha | Hakutoa mrejesho kabisa |

SAMPLE TASKS

KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA (LISTENING & SPEAKING )

| UPEO (SCOPE) | KIWANGO CHA UTENDAJI (PERFORMANCE LEVELS) |
|---|---|
| 8-10 | 4 |
| 5-7 | 3 |
| 3-4 | 2 |
| 1-2 | 1 |

## ZOEZI LA 2

## Vipengele vya Kutathmini Kuzungumza

| Kipengele | Maelezo | Viwango vya Ufanisi |
|---|---|---|
| 1. **Ufasaha wa Lugha** | Hutumia maneno sahihi, sentensi kamili, na matamshi bora. | - Hakosei sarufi wala matamshi. |
| 2. **Ushiriki wa mawasiliano** | Anaweza kushiriki kikamilifu katika mazungumzo, mjadala au mahojiano. | - Hujibu kwa hoja, huuliza maswali, hushirikiana na wengine. |
| 3. **Utaratibu na mtiririko wa mawazo** | Anaeleza hoja kwa mpangilio unaoeleweka. | - Hoja zinafuatana kwa mantiki. |
| 4. **Matumizi ya sauti na lafudhi** | Hurekebisha sauti kulingana na hisia na mazingira. | - Hutumia lafudhi ya Kiswahili sanifu, si ya kikabila. |
| 5. **Ujasiri na usemi wa mwili** | Anaonyesha kujiamini na kutumia ishara zinazosaidia uelewa. | - Husema bila hofu, hudumisha mawasiliano ya macho. |
| 6. **Adabu ya mazungumzo** | Huheshimu wenzake na kutumia lugha ya staha. | - Hupisha wengine, hutumia heshima na busara. |

KUZUNGUMZA (SPEAKING TASK )

| UPEO (SCOPE) | KIWANGO CHA UTENDAJI (PERFORMANCE LEVELS) |
|---|---|
| 16-20 | 4 |
| 11-15 | 3 |
| 6-10 | 2 |
| 1-5 | 1 |

SAMPLE TASKS

**MWONGOZO WA KUTATHMINIA KUZUNGUMZA (RUBRIKI)**

| Kipengele | Maelezo ya Kinachotathminiwa | 5 (Bora sana) | 4 (Nzuri) | 3 (Wastani) | 2 (Duni) | 1 (Haitoshi) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **1. Ufasaha wa Lugha** | Matumizi sahihi ya maneno, sarufi, na matamshi | Lugha safi na sahihi | Makosa machache | Makosa yanayoonekana | Makosa mengi | Lugha isiyoeleweka |
| **2. Mpangilio wa mawazo** | Mantiki na uhusiano wa hoja | Mawazo yamepangwa vyema | Mawazo yanafuatana | Mpangilio wa kawaida | Mpangilio hafifu | Hakuna mpangilio |
| **3. Ujasiri na sauti** | Kujiamini, sauti na lafudhi | Hujiamini na hutumia sauti bora | Hujiamini kiasi | Huchechemea | Hupoteza ujasiri | Hanyamazi au anasita sana |
| **4. Matumizi ya lugha ya staha** | Lugha ya adabu na heshima | Hutumia lugha ya staha kila mara | Wakati mwingine hutumia staha | Staha ya kawaida | Hutumia maneno yasiyofaa | Lugha ya matusi au dharau |
| **5. Ushiriki wa mawasiliano** | Kushirikiana, kuuliza, kujibu, na kuendeleza hoja | Hushiriki kikamilifu | Hushiriki mara nyingi | Ushiriki wa wastani | Ushiriki mdogo | Hashiriki kabisa |

SAMPLE TASKS

## ZOEZI LA 3
## MWONGOZO WA KUTATHMINIA KUANDIKA

Lengo kuu ni **kuchunguza uwezo wa mwanafunzi kuwasilisha mawazo kwa maandishi** kwa kutumia lugha ya Kiswahili sanifu, kwa uwazi, mpangilio, ubunifu na ufasaha.

### Vipengele Vikuu vya Tathmini

| Kipengele | Maelezo ya Kinachotathminiwa | Viwango vya Ufanisi (Alama 1–5) |
|---|---|---|
| **1. Maudhui (Ujumbe)** | Uhusiano wa mawazo na mada iliyotolewa; kina cha hoja na uthibitisho wake. | 5 = Mawazo ya kina, sahihi na yanayohusiana na mada.<br>4 = Mawazo mazuri na yanayohusiana na mada.<br>3 = Mawazo ya kawaida, mengine nje ya mada.<br>2 = Mawazo machache au dhaifu.<br>1 = Hakuna uhusiano na mada. |
| **2. Mpangilio wa Mawazo** | Ufuatiliaji wa mtiririko wa hoja (utanzu, aya, mwanzo, kati, mwisho). | 5 = Mpangilio mzuri, unaofuata mantiki.<br>4 = Mpangilio mzuri kiasi.<br>3 = Mpangilio wa wastani.<br>2 = Mpangilio hafifu.<br>1 = Hakuna mpangilio. |
| **3. Matumizi ya Lugha** | Usahihi wa sarufi, miundo ya sentensi, na maneno. | 5 = Lugha safi na sanifu.<br>4 = Makosa machache yasiyoathiri maana.<br>3 = Makosa ya kawaida yanayoonekana.<br>2 = Makosa mengi yanayochafua maana.<br>1 = Lugha isiyoeleweka. |
| **4. Msamiati (maneno)** | Ubunifu na wingi wa msamiati unaotumika kufikisha maana. | 5 = Msamiati mpana na wa kisanaa.<br>4 = Msamiati mzuri.<br>3 = Msamiati wa kawaida.<br>2 = Msamiati mdogo au unaorudiwa.<br>1 = Msamiati hafifu au usiofaa. |
| **5. Mtindo na Ufasaha** | Urembo wa uandishi – matumizi ya taswira, jazanda, hisia, na ubunifu. | 5 = Mtindo wa kuvutia na wa kisanaa.<br>4 = Mtindo mzuri.3 = Mtindo wa kawaida.<br>2 = Mtindo hafifu.<br>1 = Hakuna urembo wa kisanaa. |

SAMPLE TASKS

| Kipengele | Maelezo ya Kinachotathminiwa | Viwango vya Ufanisi (Alama 1–5) |
|---|---|---|
| **6. Umbo la maandishi** | Usafi wa maandiko, alama za uakifishaji, herufi kubwa/ndogo, na mwandiko. | 5 = Safi, sahihi na unaosomeka vizuri.<br>4 = Safi kiasi.<br>3 = Makosa ya uandishi yanayoonekana.<br>2 = Machache yasiyoeleweka.<br>1 = Mwandiko usioeleweka. |

**Ufasiri wa Viwango vya Alama Jumla**

**KUANDIKA (WRITING TASK )**

| UPEO (SCOPE) | KIWANGO CHA UTENDAJI (PERFORMANCE LEVELS) |
|---|---|
| 16-20 | 4 |
| 11-15 | 3 |
| 6-10 | 2 |
| 1-5 | 1 |

## ZOEZI LA 4: TAFSIRI

## JIBU LINALOTARAJIWA

**TAFSIRI**

Ajali za barabarani ni chanzo kikuu cha majeraha na vifo duniani. Mojawapo ya sababu kuu ni uendeshaji mbaya wa magari kama vile mwendo wa kasi kupita kiasi, kuyapita magari mengine kwa njia hatari, na kutokufuata sheria za barabarani. Ajali nyingi pia hutokea kutokana na ulevi wa madereva, ambapo hushindwa kudhibiti magari kwa sababu ya kuhisi vibaya au kupoteza umakini. Sababu nyingine ni matumizi ya simu wakati wa kuendesha gari, jambo linalosababisha madereva kutokuzingatia barabara. Hali mbaya ya barabara kama mashimo na ukosefu wa alama sahihi za barabarani pia huchangia ajali. Aidha, magari yasiyokuwa katika hali nzuri na kushindwa kuyatunza ipasavyo yanaweza kusababisha hitilafu za kiufundi zinazoleta ajali.

Ili kuzuia ajali za barabarani, madereva na mamlaka husika wanapaswa kushirikiana. Madereva wanapaswa kufuata sheria za barabarani, kuepuka mwendo wa kasi, na kutoendesha wakiwa wamelewa pombe au dawa za kulevya. Pia wanapaswa kuhakikisha magari yao yako katika hali nzuri na kuwa makini wanapokuwa barabarani. Kwa upande mwingine, mamlaka zinapaswa kutengeneza barabara ipasavyo, kuweka alama wazi, na kutekeleza sheria kwa ukali. Kampeni za uhamasishaji kuhusu usalama barabarani zinaweza kusaidia kubadilisha mitazamo hasi. Kwa kushirikiana kwa uwajibikaji, idadi ya ajali inaweza kupunguzwa kwa kiasi kikubwa na barabara kuwa salama kwa wote.

SAMPLE TASKS

**WONGOZO WA KUTATHMINIA VIPENGELE VYA TAFSIRI**

**1. Ufasaha wa Lugha**

**Maelezo:** Uwezo wa mtafsiri kutumia lugha lengwa kwa njia sahihi na inayoeleweka.

**Vigezo vya kutathmini:**

| Kiwango | Maelezo |
|---|---|
| 5 | Lugha fasaha, sahihi, na mtiririko wa asili. |
| 4 | Lugha ni nzuri, makosa machache ya kisarufi au mtindo. |
| 3 | Makosa yanayoonekana lakini maana bado inaeleweka. |
| 2 | Lugha imevurugika kiasi, uelewekaji ni wa shida. |
| 1 | Lugha si sahihi, tafsiri haiwezi kueleweka. |

**2. Uaminifu kwa Maana ya Asili**

**Maelezo:** Kiwango ambacho tafsiri inabeba maana, hisia, na dhamira ya maandishi chanzi.
**Vigezo vya kutathmini:**

| Kiwango | Maelezo |
|---|---|
| 5 | Maana ya asili imehifadhiwa kikamilifu. |
| 4 | Mabadiliko madogo yasiyoathiri ujumbe mkuu. |
| 3 | Baadhi ya maana zimepotea au kubadilika kiasi. |
| 2 | Ujumbe wa asili umevurugika. |
| 1 | Tafsiri imepoteza maana kabisa. |

**3. Ulinganifu wa Mitindo**

**Maelezo:** Kudumisha mtindo, msamiati, na sauti ya mwandishi wa asili.
**Vigezo vya kutathmini:**

| Kiwango | Maelezo |
|---|---|
| 5 | Mtindo wa asili umehifadhiwa ipasavyo. |
| 4 | Mtindo unakaribia ule wa asili. |
| 3 | Tofauti dhahiri za kimtindo zipo. |
| 2 | Mtindo umebadilika sana. |
| 1 | Hakuna dalili ya mtindo wa asili. |

SAMPLE TASKS

**4. Ufasiri wa Tamathali za Lugha na Mifumo ya Utamaduni**

**Maelezo:** Uelewa wa mtafsiri kuhusu tamathali, methali, misemo, na vipengele vya kitamaduni.
**Vigezo vya kutathmini:**

| Kiwango | Maelezo |
|---|---|
| 5 | Tamathali na misemo zimetafsiriwa kwa usahihi na ubunifu. |
| 4 | Tafsiri nzuri ila baadhi ya tamathali zimepoteza nguvu yake. |
| 3 | Tamathali kadhaa zimeachwa au kubadilishwa vibaya. |
| 2 | Uelewa mdogo wa kipengele cha kitamaduni. |
| 1 | Tafsiri ya moja kwa moja isiyo na maana. |

**5. Muundo na Mpangilio wa Sentensi**

**Maelezo:** Mpangilio wa sentensi na aya katika lugha lengwa.
**Vigezo vya kutathmini:**

| Kiwango | Maelezo |
|---|---|
| 5 | Sentensi zimepangwa vizuri na mtiririko wa mawazo ni mzuri. |
| 4 | Mpangilio mzuri kwa ujumla. |
| 3 | Baadhi ya sentensi hazina mpangilio bora. |
| 2 | Muundo umepotea kiasi. |
| 1 | Sentensi hazina maana au mpangilio. |

**6. Ubunifu na Ustadi wa Mtafsiri**

**Maelezo:** Uwezo wa kutumia maarifa ya lugha na utamaduni ili kutoa tafsiri ya kuvutia na sahihi.
**Vigezo vya kutathmini:**

| Kiwango | Maelezo |
|---|---|
| 5 | Tafsiri ya kitaalamu, yenye ubunifu na mvuto. |
| 4 | Tafsiri ya kitaalamu, lakini ubunifu mdogo. |
| 3 | Inayoonyesha jitihada za ubunifu. |

SAMPLE TASKS

| Kiwango | Maelezo |
|---|---|
| 2 | Ubunifu ni hafifu. |
| 1 | Tafsiri kavu na isiyochangamsha. |

**7. Matumizi Sahihi ya Msamiati**

**Maelezo:** Uteuzi wa maneno yanayofaa katika muktadha.
**Vigezo vya kutathmini:**

| Kiwango | Maelezo |
|---|---|
| 5 | Msamiati sahihi, unaofaa muktadha na hadhira. |
| 4 | Makosa machache yasiyoathiri ujumbe. |
| 3 | Makosa kadhaa ya uteuzi wa maneno. |
| 2 | Msamiati usio sahihi mara nyingi. |
| 1 | Maneno mengi hayafai kabisa. |

**Mfumo wa Alama (jumla ya alama 10)**

| Kipengele | Alama za juu |
|---|---|
| Ufasaha wa lugha | 1 |
| Uaminifu kwa maana ya asili | 2 |
| Ulinganifu wa mitindo | 2 |
| Ufasiri wa tamathali na utamaduni | 1 |
| Muundo wa sentensi | 1 |
| Ubunifu wa mtafsiri | 1 |
| Msamiati sahihi | 1 |
| **JUMLA** | 10 |

**TAFSIRI (TRANSLATION)**

| UPEO (SCOPE) | KIWANGO CHA UTENDAJI (PERFORMANCE LEVELS) |
|---|---|
| 8-10 | 4 |
| 5-7 | 3 |
| 3-4 | 2 |
| 1-2 | 1 |

SAMPLE TASKS

**FOMU YA TATHMINI YA TAFSIRI**

**Jina la Mwanafunzi: ____________________________**
**Gredi: ____________**
**Tarehe: ______________**
**Kazi ya Tafsiri Kutoka: ____________________________**
**Kuelekea: ____________________________**

**A. VIPENGELE VYA TATHMINI**

| Na. | Kipengele cha Tathmini | Maelezo ya Kiwango cha Ubora | Alama (1–5) | Maoni ya Mwalimu |
|---|---|---|---|---|
| 1 | **Ufasaha wa Lugha** | Matumizi bora ya sarufi, muundo wa sentensi na mtiririko wa lugha fasaha. | ____ | ____________________________ |
| 2 | **Uaminifu kwa Maana ya Asili** | Ujumbe, hisia na dhamira ya maandishi chanzi yamehifadhiwa ipasavyo. | ____ | ____________________________ |
| 3 | **Ulinganifu wa Mitindo** | Mtindo na toni ya maandiko ya asili yameendelezwa katika tafsiri. | ____ | ____________________________ |
| 4 | **Ufasiri wa Tamathali na Vipengele vya Utamaduni** | Tamathali, methali, na misemo imetafsiriwa kwa usahihi na uhalisia. | ____ | ____________________________ |
| 5 | **Muundo na Mpangilio wa Sentensi** | Mpangilio wa mawazo, aya, na sentensi unaeleweka vizuri. | ____ | ____________________________ |
| 6 | **Ubunifu na Ustadi wa Mtafsiri** | Uwezo wa kutumia maarifa ya lugha na ubunifu kutafsiri kwa mvuto. | ____ | ____________________________ |
| 7 | **Matumizi Sahihi ya Msamiati** | Maneno yaliyotumika yanafaa muktadha na hadhira. | ____ | ____________________________ |

SAMPLE TASKS

**C. MAONI YA MWALIMU**

**Sahihi ya Mwalimu: ______________________**

**Tarehe: ______________________**

# ZOEZI LA 5

a) **Ufupisho wa matini (maneno 65):**

Ajali za barabarani husababishwa na mwendo wa kasi, ulevi wa madereva, matumizi ya simu, barabara mbovu, na magari yasiyotunzwa vizuri. Ili kuzuia ajali, madereva wanapaswa kufuata sheria, kuepuka ulevi na kuhakikisha magari yako salama. Serikali inapaswa kutengeneza barabara, kuweka alama wazi, na kuelimisha wananchi kuhusu usalama barabarani ili kupunguza ajali.

**(Maneno 50)**

**Msimamo wa mwandishi (maneno 20):**
Mwandishi anaamini kuwa usalama barabarani unategemea ushirikiano kati ya madereva na serikali katika kutekeleza wajibu wao ipasavyo.

**(Maneno 17)**

## MWONGOZO WA KUTATHMINIA UFUPISHO

**1. Uelewa wa Maudhui (Maana ya Kifungu)**

**Maelezo:** Mwanafunzi anaonyesha uelewa wa ujumbe, hoja kuu na dhamira ya maandiko ya chanzo.
**Vigezo vya kutathmini:**

| Kiwango | Maelezo |
|---|---|
| 5 | Ameelewa vizuri ujumbe wote muhimu wa kifungu. |
| 4 | Ameelewa ujumbe mkuu, ingawa baadhi ya hoja ndogo zimeachwa. |
| 3 | Ameelewa kwa sehemu tu; baadhi ya hoja zimekosekana. |
| 2 | Uelewa ni mdogo; amepoteza maana kuu. |
| 1 | Hakuelewa kabisa kifungu chanzi. |

---

**2. Uchaguzi wa Mawazo Muhimu**

**Maelezo:** Uwezo wa mwanafunzi kubainisha hoja kuu na kuacha maelezo madogo yasiyo muhimu.
**Vigezo vya kutathmini:**

| Kiwango | Maelezo |
|---|---|
| 5 | Amechagua hoja kuu zote kwa usahihi. |
| 4 | Hoja nyingi kuu zimechaguliwa, chache zimeachwa. |
| 3 | Baadhi ya hoja kuu zimekosekana au zisizo muhimu zimejumuishwa. |
| 2 | Hoja kuu zimechanganyika na maelezo madogo. |
| 1 | Hakutofautisha hoja kuu na maelezo madogo. |

SAMPLE TASKS

### 3. Ufasaha wa Lugha

**Maelezo:** Matumizi ya lugha fasaha, sarufi sahihi na mtiririko wa mawazo unaoeleweka.
**Vigezo vya kutathmini:**

| Kiwango | Maelezo |
|---|---|
| 5 | Lugha safi, sahihi na yenye mtiririko bora. |
| 4 | Lugha nzuri, makosa madogo ya kisarufi. |
| 3 | Makosa ya sarufi yanayoonekana lakini maana inaeleweka. |
| 2 | Lugha imevurugika kiasi, uelewekaji ni wa shida. |
| 1 | Lugha si sahihi, haieleweki. |

---

### 4. Urefu Unaofaa

**Maelezo:** Ufupisho unafuata idadi ya maneno au mistari iliyotakiwa (kwa mfano, maneno 65 au 100).
**Vigezo vya kutathmini:**

| Kiwango | Maelezo |
|---|---|
| 5 | Amezingatia kikamilifu idadi ya maneno/mistari iliyoagizwa. |
| 4 | Amevuka au kupunguza kwa tofauti ndogo. |
| 3 | Tofauti kubwa kidogo kwenye idadi ya maneno. |
| 2 | Tofauti kubwa inayodhihirisha kutozingatia maagizo. |
| 1 | Hakufuata kabisa idadi iliyotakiwa. |

---

### 5. Ulinganifu na Mpangilio wa Mawazo

**Maelezo:** Mawazo yamepangwa kwa utaratibu unaoonyesha mtiririko wa hoja kutoka mwanzo hadi mwisho.
**Vigezo vya kutathmini:**

| Kiwango | Maelezo |
|---|---|
| 5 | Mpangilio mzuri, mawazo yanajenga hoja kwa ufasaha. |
| 4 | Mawazo yanafuatana vizuri ingawa kuna mapungufu madogo. |
| 3 | Mawazo yanafuatana kwa shida, mtiririko si mzuri. |
| 2 | Mpangilio umevurugika. |
| 1 | Hakuna utaratibu wa mawazo. |

SAMPLE TASKS

**6. Uaminifu kwa Maana ya Asili**

**Maelezo:** Ufupisho unahifadhi maana ya maandiko ya chanzo bila kuongeza au kubadilisha.
**Vigezo vya kutathmini:**

| Kiwango | Maelezo |
|---|---|
| 5 | Maana ya asili imehifadhiwa kikamilifu. |
| 4 | Mabadiliko madogo yasiyoathiri ujumbe mkuu. |
| 3 | Baadhi ya maana zimepotea au kubadilika. |
| 2 | Ujumbe wa asili umevurugika. |
| 1 | Maana imepotea kabisa. |

---

**MFUMO WA ALAMA (JUMLA YA ALAMA 10)**

| Kipengele | Alama za Juu |
|---|---|
| Uelewa wa maudhui | 2 |
| Uchaguzi wa mawazo muhimu | 2 |
| Ufasaha wa lugha | 2 |
| Urefu unaofaa | 2 |
| Ulinganifu wa mawazo | 1 |
| Uaminifu kwa maana ya asili | 1 |
| **JUMLA** | 10 |

**UFUPISHO (SUMMARY WRITING)**

| UPEO (SCOPE) | KIWANGO CHA UTENDAJI (PERFORMANCE LEVELS) |
|---|---|
| 8-10 | 4 |
| 5-7 | 3 |
| 3-4 | 2 |
| 1-2 | 1 |

SAMPLE TASKS

**FOMU YA TATHMINI YA UFUPISHO**
**Jina la Mwanafunzi: ___________________________**
**Gredi: ____________**
**Tarehe: ______________**
**Kifungu Chanzo: __________________________________________**
**Idadi ya Maneno Iliyotakiwa: ____________**
**Idadi ya Maneno Halisi: ____________**

**A. VIPENGELE VYA TATHMINI**

| Na. | Kipengele cha Tathmini | Maelezo ya Kiwango cha Ubora | Alama (1–5) | Maoni ya Mwalimu |
|---|---|---|---|---|
| **1** | **Uelewa wa Maudhui** | Ameonyesha uelewa kamili wa maana na ujumbe wa kifungu chanzi. | ____ | ___________________________ |
| **2** | **Uchaguzi wa Mawazo Muhimu** | Amebainisha hoja kuu pekee na kuacha maelezo yasiyo muhimu. | ____ | ___________________________ |
| **3** | **Ufasaha wa Lugha** | Lugha sahihi, yenye mtiririko na sarufi bora. | ____ | ___________________________ |
| **4** | **Urefu Unaofaa** | Amezingatia idadi ya maneno au mistari iliyotolewa. | ____ | ___________________________ |
| **5** | **Ulinganifu na Mpangilio wa Mawazo** | Mawazo yamepangwa kwa utaratibu unaoeleweka. | ____ | ___________________________ |
| **6** | **Uaminifu kwa Maana ya Asili** | Tafsiri fupi haijabadilisha maana ya maandiko ya chanzo. | ____ | ___________________________ |

**B. MUHTASARI WA MATOKEO**

| **Kipengele** | **Alama Zilizopatikana** | **Alama za Juu** |
|---|---|---|
| Jumla ya Alama | ______ | |

**C. MAONI YA MWALIMU**

______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

**Sahihi ya Mwalimu: _____________________**
**Tarehe: _____________________**

SAMPLE TASKS

# ZOEZI LA 6: KUHARIRI MATINI

**Matini iliyosahihishwa:**
Ajali za barabarani husababishwa na mwendo wa kasi, ulevi wa madereva, na matumizi ya rununu wakati wa kuendesha gari. Barabara nyingi ni mbovu kutokana na serikali kushindwa kuzitengeneza ipasavyo. Madereva wanapaswa kufuata sheria na kuhakikisha magari yao yako katika hali nzuri. Serikali inafaa kuweka alama za barabarani kwa uwazi na kuelimisha wananchi kuhusu usalama barabarani ili kupunguza ajali ambazo husababisha vifo vingi kila siku. Wajibu wangu katika kuhakikisha usalama barabarani ni kufuata sheria za barabarani na kuwa mwangalifu ninapotumia barabara.

# MWONGOZO WA KUTATHMINIA UHARIRI WA MATINI

### 1. Uelewa wa Maudhui ya Matini Asilia

**Maelezo:** Mwanafunzi anaonyesha kuelewa vizuri maudhui, dhamira, na ujumbe wa matini kabla ya kuhariri.
**Vigezo vya kutathmini:**

| Kiwango | Maelezo |
|---|---|
| 5 | Ameelewa kwa kina maudhui na madhumuni ya matini. |
| 4 | Ameelewa ujumbe mkuu vizuri, makosa madogo tu. |
| 3 | Uelewa wa wastani, baadhi ya maana zimepotea. |
| 2 | Uelewa mdogo; mwelekeo wa matini umevurugika. |
| 1 | Hakuelewa kabisa maana ya matini asilia. |

### 2. Utambuzi wa Makosa

**Maelezo:** Uwezo wa kubaini makosa yaliyomo katika matini (kisarufi, kimatamshi, kimtindo, au kiupangaji).
**Vigezo vya kutathmini:**

| Kiwango | Maelezo |
|---|---|
| 5 | Amebaini kwa usahihi makosa yote muhimu. |
| 4 | Makosa mengi yamebainishwa, baadhi yameachwa. |
| 3 | Makosa ya msingi yamebainishwa lakini mengine yameachwa. |
| 2 | Makosa machache tu yamegunduliwa. |
| 1 | Hakutambua makosa muhimu. |

SAMPLE TASKS

### 3. Uboreshaji wa Lugha

**Maelezo:** Uwezo wa kutumia lugha sahihi, yenye ufasaha na mtiririko baada ya kuhariri.
**Vigezo vya kutathmini:**

| Kiwango | Maelezo |
|---|---|
| **5** | Matini iliyohaririwa ina lugha safi, sahihi na fasaha. |
| **4** | Makosa machache ya kisarufi au kimuundo. |
| **3** | Makosa yanayoonekana lakini maana inabaki wazi. |
| **2** | Lugha ina dosari nyingi. |
| **1** | Matini imevurugika, haieleweki. |

---

### 4. Ulinganifu wa Mtindo na Mpangilio

**Maelezo:** Kudumisha mtindo wa uandishi wa asili huku akiboresha mpangilio wa mawazo.
**Vigezo vya kutathmini:**

| Kiwango | Maelezo |
|---|---|
| **5** | Mtindo wa asili umehifadhiwa na umeboreshwa vizuri. |
| **4** | Mtindo unaendana kwa kiasi kikubwa na ule wa asili. |
| **3** | Baadhi ya mabadiliko yamepoteza mtindo wa awali. |
| **2** | Mtindo umebadilika sana. |
| **1** | Hakuna ulinganifu wa mtindo kabisa. |

### 5. Ufasiri wa Maana na Ujumbe

**Maelezo:** Baada ya kuhariri, maana na dhamira ya matini inabaki wazi na sahihi.
**Vigezo vya kutathmini:**

| Kiwango | Maelezo |
|---|---|
| **5** | Maana na ujumbe wa asili umehifadhiwa kikamilifu. |
| **4** | Mabadiliko madogo yasiyoathiri ujumbe. |
| **3** | Maana zingine zimepotea au kubadilika kiasi. |
| **2** | Ujumbe umevurugika. |
| **1** | Maana imepotea kabisa. |

SAMPLE TASKS

**6. Ubunifu katika Uhariri**

**Maelezo:** Uwezo wa mwanafunzi kuboresha matini kwa njia bunifu (kuchagua maneno bora, kuongeza muundo wa kitaalamu, n.k.).
**Vigezo vya kutathmini:**

| Kiwango | Maelezo |
|---|---|
| 5 | Uhariri wa kitaalamu, wenye ubunifu na ubora wa juu. |
| 4 | Uhariri mzuri, lakini ubunifu ni wa wastani. |
| 3 | Kuna juhudi za ubunifu ingawa si thabiti. |
| 2 | Uhariri wa kawaida bila ubunifu. |
| 1 | Hakuna ubunifu wala uboreshaji. |

---

**MFUMO WA ALAMA (JUMLA YA ALAMA 30)**

| Kipengele | Alama za Juu |
|---|---|
| Uelewa wa maudhui | 2 |
| Utambuzi wa makosa | 2 |
| Uboreshaji wa lugha | 2 |
| Ulinganifu wa mtindo | 2 |
| Ufasiri wa maana | 1 |
| Ubunifu katika uhariri | 1 |
| **JUMLA** | **10** |

SAMPLE TASKS

## KUHARIRI MATINI (TEXT EDITING)

| UPEO (SCOPE) | KIWANGO CHA UTENDAJI (PERFORMANCE LEVELS) |
|---|---|
| 8-10 | 4 |
| 5-7 | 3 |
| 3-4 | 2 |
| 1-2 | 1 |